**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU FURSA YA UFADHILI WA MASOMO KWA WANACHUO WA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU MAALUMU KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

## 1.0 UTANGULIZI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatangaza fursa ya Ufadhili wa Masomo ngazi ya **Stashahada ya Ualimu wa Elimu Maalumu**. Maombi yanakaribishwa kwa wanachuo wanaosoma, Stashahada ya Elimu maalumu katika maeneo yafuatayo: **Ulemavu wa Akili, Usonji, Uziwi, Uziwi Kutoona na Ulemavu wa Uoni.**

## 2.0 SIFA ZA KUPATA UFADHILI

Ufadhili huu utatolewa kwa wanafunzi wenye sifa zifuatazo:

a) Awe Mtanzania;

b) Awe amepata udahili katika Chuo cha Ualimu kinachotambulika na Serikali na kinatoa Stashahada ya Ualimu Elimu Maalumu;

## 3.0 NAKALA ZA KUWASILISHA

i Barua ya kuomba ufadhili ikionesha kozi unayosoma, namba ya simu na barua pepe;

ii Nakala ya vyeti vya kitaaluma vilivyothibitishwa na mwanasheria;

iii Cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na mwanasheria; na

iv Barua kutoka kwa Mkuu wa Chuo ikionesha kuwa umedahiliwa katika Chuo husika.

## 4.0 MAENEO YA UFADHILI

Ufadhili utahusisha maeneo yafuatayo:

a) Ada ya Mafunzo;

b) Michango mingine ya Chuo (Mf. Ulinzi,ukarabati n.k);

c) Vifaa vya kufundishia na kujifunzia;

d) Nauli; na

e) Bima ya Afya.

## 5.0 MASHARTI YA UFADHILI

Mwanachuo atakayepata ufadhili kwa ajili ya kusoma Stashahada ya Elimu Maalumu atawajibika kuzingatia masharti yafuatayo:

a) Anapaswa kusoma, kuelewa na kusaini Mkataba wa Makubaliano ya Ufadhili wa Masomo kati yake na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;

b) Anapaswa kuwa na akaunti ya Benki kwa ajili ya fedha atakazolipwa moja kwa moja;

c) Mnufaika hataruhusiwa kubadilisha programu ya masomo aliyopatia ufadhili bila idhini ya Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;

d) Mnufaika hataruhusiwa kuahirisha masomo, isipokuwa kwa sababu za kiafya, na kuthibitishwa na Daktari kutoka katika Kituo cha Afya au Hospitali inayotambuklika na Serikali;

e) Ikiwa mnufaika ataghairi fursa ya ufadhili, atapaswa kutoa taarifa kwa maandishi kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia kwa Mkuu wa chuo alichodahiliwa na kujisajili.

## 6.0 MUDA WA UFADHILI

Ufadhili huu ni kwa kipindi cha miaka miwili (02) ya masomo kwa wanachuo watakaokidhi vigezo viliyobainishwa katika kipengele Na. 5.

## 7.0 UTARATIBU WA KUOMBA UFADHILI

Maombi yawasilishwe Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ndani ya siku 15 kuanzia Agosti 18 hadi 28, 2025. Maombi yatumwe kwa **Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, S.L.P 10 Dodoma.** Orodha ya Wanachuo watakaokuwa wamepata ufadhili huo itawekwa katika tovuti ya Wizara (www.moe.go.tz).

**Imetolewa na:**

**Katibu Mkuu**

**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

**Agosti, 2025**